

TAARIFA YA KATIBU MKUU OFISI YA RAIS IKULU, BW. MULULI MAHENDEKA, KWA MHE. RIDHIWANI KIKWETE (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA SITA (6) CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 19 FEBRUARI, 2026 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA

Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb); Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

Mhe. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria

Makatibu Wakuu wote,

Dkt. Mussa Kisaka; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),

Mhandisi. Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo/Sehemu, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;

Viongozi wa Dini,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kwa muda wa siku tatu tulizokuwa hapa.

Vilevile napenda kukushukuru **Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb)**, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kutenga muda na kuweza kuwa nasi hii leo, katika hafla ya kufunga Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao. Aidha, nakushukuru kwa jitihada zako hasa miongozo na maelekezo kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Mhe. Waziri,

Kikao Kazi hiki kimeainisha kwa uwazi vipaumbele muhimu katika kuimarisha maendeleo ya Serikali Mtandao, ikiwemo uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo, kuunganisha mifumo ya TEHAMA Serikalini, kuimarisha usalama wa taarifa za Serikali, pamoja na kujenga uwezo wa rasilimali watu katika taasisi za umma kupitia mafunzo ya ubobezi katika fani ya TEHAMA.

Katika muktadha huo, napenda kuahidi kuwa, nikiwa **Katibu Mkuu** mwenye dhamana ya kuisimamia e-GA katika utekelezaji wa maazimio haya na maelekezo mengine utakayotoa kuhusu utekelezaji wa Serikali Mtandao, nitaendelea:

- Kuboresha Kanuni na miongozo inayohusu utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao;
- Kuisimamia na kuratibu kwa karibu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

- ;
- Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini kwa mujibu wa Sheria na viwango vilivyopo;
- Kujenga uwezo wa rasilimali watu, ikiwemo mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wanaosimamia mifumo ya TEHAMA Serikalini, kutokana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani;
- Na kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi na maazimio yaliyofikiwa.

Mhe. Waziri,

Napenda kutoa wito kwa Wakuu wa Taasisi zote kuhakikisha wanashirikiana kwa karibu na e-GA, na kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na viongozi katika kikao hiki, ili kufikia lengo la kuwa na Serikali Mtandao inayotoa huduma bora kwa wananchi, zilizo salama na jumuishi.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru washiriki wote kwa mchango wao, Wadhamini kwa kujitoa kwa hali na mali, watoa mada pamoja na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa uratibu mzuri wa kikao kazi hiki.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Kazi na Utu....